TANGAZO LA SERIKALI NA. 207 la tarehe 28/3/2025

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)
(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 153(1)(b))*

SHERIA NDOGO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA UDHIBITI NA USIMAMIZI WA MIFUGO YA HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE YA MWAKA 2025

Jina

TS Na. 487 la 2024

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Udhibiti na Usimamizi wa Mifugo ya Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ya Mwaka 2025, na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya Udhibiti na Usimamizi wa Mifugo ya Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ya Mwaka 2024 ambayo katika Sheria Ndogo hii inarejewa kama “Sheria Ndogo kuu”.

Marekebisho ya kanuni ya 3

2. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 3 kwa kuongeza tafsiri ya msamiati mpya ufuatao kwa kuzingatia mtiririko wa kialfabeti:

> ““mpango bora wa matumizi ya ardhi” maana yake ni mpangilio mzuri wa matumizi ya ardhi kwa kuzingatia maendeleo endelevu, ufanisi wa rasilimali, na mahitaji ya sasa na ya baadaye ya jamii;”.

Marekebisho ya kanuni ya 8

3. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 8 kwa kufuta kanuni ndogo ya (4) na badala yake kuweka kanuni ndogo ifuatayo:

"(4) Halmashauri, ndani ya siku tatu kabla ya kuuza mfugo kwa mnada itamjulisha mmiliki na umma kuhusu kusudio hilo kwa njia ya matangazo ya maandishi au mdomo kadiri itakavyoonekana inafaa.".

Dodoma,
10 Januri, 2025

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi-OR-TAMISEMI*